

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE  
30/12/2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

- |                       |              |
|-----------------------|--------------|
| 1. Kedmon Chipanyanga | - Mwenyekiti |
| 2. Chaina Masamaki    | - Katibu     |
| 3. Edward J. Mturi    | - Mjumbe     |
| 4. Karani Ruhumbika   | -Mjumbe      |
| 5. Josiah P.Saoke     | -Mjumbe      |

**WAALIKWA.**

- |                         |                           |
|-------------------------|---------------------------|
| 1. Alfaxad M. Kizinga   | - Kaimu Mwanasheria(W)    |
| 2. Bhoke Chacha         | - Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 3. Dr. Deusdedit Kalosa | - Mganga Mkuu wa Wilaya   |
| 4. Wumbe Harun          | - Kaimu Mweka hazina(W)   |
| 5. Rehema Mdoe          | - Afisa Utumishi (w)      |

**SEKRETARIETI.**

1. Robert Makendo
2. Poul J. Mataba
3. Paschal Samson

**AGENDA ZA KIKAO.**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma muhtasari wa kikao kilichopita.
4. Kujadili na kuidhinisha Ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa dharura katika Hopsitali ya Wilaya ya Butiama na Nyumba ya Mtumishi kituo cha Afya Kirumi.
5. Mengineyo.
6. Kufunga kikao.

**CTB/2021/2022/04: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa nane na dakika kumi na tano (08:15) alasiri kwa kuwakaribisha wajumbe waliohuduria na kuwaomba kuchangia kwa umakini ili kuwezesha maombi yaliyo mbele ya kikao kuidhinishwa kutekelezwa haraka na kwa ufanisi kwa manufaa ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

### **CTB/2021/2022/05: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Jumla ya agenda sita zilisomwa na Katibu wa Bodi ya Zabuni na zikathhibitishwa na kujadiliwa na wajumbe wote waliohuduria katika kikao.

### **CTB/2021/2022/06: KUSOMA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.**

Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 03-09-2021 ulisomwa, ukajadiliwa/ukasahihishwa na ukakubalika kuwa kumbukumbu halali ya kikao.

### **CTB/2021/2022/07: KUJADILI NA KUIDHINISHA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA KATIKA HOSIPITALI YA WILAYA YA BUTIAMA NA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA KITUO CHA AFYA KIRUMI.**

Katibu wa wa Bodi ya zabuni aliwasilisha maombi ya kuidhinisha kazi ya ujenzi wa jengo la dharura katika Hospitali mpya ya Wilaya ya Butiama Tsh. 300,000,000.00 na nyumba ya mtumishi katika kituo cha Afya Kirumi Tsh. 90,000,000.00 kama ilivyoombwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (DMO), na fedha ya miradi hiyo ni kutoka "IMF" na tayari iko kwenye akaunti ya Hospitali ya wilaya ya Butiama.

Pamoja na maombi hayo, pia Katibu alisema kuna maelekezo kutoka OR-TAMISEMI yanayoelekeza kwamba ujenzi huo ufanyike kwa kutumia Mkandarasi, na kufikia tarehe 31/12/2021 mchakato wa manunuzi uwe umekamilisha hatua ya kuaini mkataba wa ujenzi wa miradi hiyo. Kabla ya mjadala kitengo cha Manunuzi kilishauri atumike mkadarasi kwa njia ya manunuzi ya "Single Source" ili kuharakisha zoezi hilo kwani njia ya manunuzi ya "Competitive tendering" itachukua muda mrefu hadi kumpata

mkandarasi na hivyo kuchelewa kwa mujibu wa maelekezo ya OR-TAMISEMI.

Wajumbe wote kwa pamoja walijadili maombi hayo na kuyapitisha yaendelee na mchakato wa manunuzi na kukubaliana kwa pamoja kuwa njia ya "Single Source" ndio itakayo tumika na pia PMU wazingatie taratibu za manunuzi.

### **CTB/2021/2022/08: MENGINEYO.**

Wajumbe walikumbushia posho yao ya kikao ambapo DMO aliahidi kuwalipa mara apatapo OC ya mwezi unaofuata.


### **CTB/2021/2022/09: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa tisa na dakika arobaini na tatu (09:43) Alasiri kwa kuwashukuru wajumbe kwa usikivu walioonesha na mijadala mizuri waliyofanya kwa maslahi mapana ya Halmashauri.

### **MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA:**

  
.....  
**MWENYEKITI**

  
.....  
**KATIBU**

  
.....  
**TAREHE**